# SAYANSI YA KUJISHUGHULISHA

KUTOKUWA NA SHUGHULI ZA KUFANYA HUFANYA WATOTO KUWA NA WASIWASI NA KUWA WAHARIBIFU. WATOTO HUSTAHIMILI VYEMA WANAPOKUWA NA SHUGHULI NYINGI ZA KUWASAIDIA WENGINE. WAZAZI WANAWEZA KUWAPA KAZI ZENYE USALAMA KAMA VILE SHUGHULI ZA MUZIKI, SANAA, UFUNDI, VITABU, NA PIA KUWAHIMIZA WATOTO KUWASILIANA NA MARAFIKI.

MARA NYINGI, WATOTO WALIO NA SHUGHULI NYINGI HUJA KUWA NA FURAHA ZAIDI KULIKO WATOTO WASIO NA SHUGHULI NYINGI.

KUWA NA SHUGHULI NYINGI KUNAPUNGUZA HATARI YA TABIA ZA USUMBUFU KAMA VILE KUTOKUWA MAKINI, UKAIDI, UCHOKOZI NA MATUMIZI YA DAWA ZA KULEVYA.

KUUNGANISHWA NA TAMADUNI NI MUHIMU KWA UKUAJI WA UBONGO WA WATOTO.

SAYANSI YA MISHIPA YA FAHAMU INAONYESHA KWAMBA KUJIFUNZA MUZIKI HUONGEZA MAENEO YA UBONGO YANAYOHUSIKA NA UCHAKATAJI WA SAUTI, UKUZAJI WA LUGHA, NA UJUZI WA KUSOMA KWA WATOTO WADOGO.

UWEZO WA KUTENGENEZA NA KUDUMU NA RAFIKI WA KARIBU JAPO MMOJA NI MUHIMU KWA USTAWI WA WATOTO. URAFIKI WA KARIBU HUSAIDIA KUPUNGUZA MSONGO WA MAWAZO NA HATA KUUPA MWILI KINGA DHIDI YA MAGONJWA YANAYOSABABISHWA NA VIRUSI.

KUOTA NDOTO ZA MCHANA KWA NJIA CHANYA KUNACHANGIA KATIKA UKUAJI WA WATOTO KIJAMII-KIHISIA NA UBUNIFU. MUDA WA PEKE YAO WENYEWE HUWAPA UWEZO WA KUFIKIRIA ULIMWENGU MWINGINE NA KUSHUGHULIKIA MATUKIO YAO YA MAISHA, AMBAYO NI MUHIMU KWA UJUZI WA KUFANYA MAAMUZI YA SIKU ZIJAZO.

TABIA YA KUTOKUJISHUGHULISHA INAHUSISHWA NA UNENE, KISUKARI CHA UTOTONI NA BAADAYE MAGONJWA YA MOYO NA MISHIPA YA DAMU.

LAKINI PIA UJUZI WA KIJAMII WA UTOTONI KAMA VILE KUSHIRIKIANA, KUSAIDIANA, NA KUFARIJI KUNA MATOKEO CHANYA KATIKA UTENDAJI WA KITAALUMA NA URAFIKI KATIKA UJANA NA MAHUSIANO NA WENGINE KATIKA UTU UZIMA.



UNODC
United Nations Office on Drugs and Crime

Kwa taarifa zaidi, tembelea:
**www.unodc.org/listenfirst**

PAKUA **APP** YA HURU

**Kwa hisani ya watu wa Ufaransa**